TANGAZO LA SERIKALI NA. 281 la tarehe 7/4/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 24(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA UPANGAJI MAALUMU LA MSEKO YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Upangaji Maalumu la Mseko ya mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Maalumu Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji maalumu kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na ya kina katika eneo la kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji maalumu lipo ndani ya mipaka ifuatayo –

“Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NP3 yenye majira - nukta 473665MS, 9391246KZ; baada ya hapo mpaka unaendelea Mashariki kwa umbali wa kilomita 7.149 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VTB 777 yenye majira - nukta 480625MS, 9392928KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 1.747 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P1 yenye majira - nukta 472289MS, 9392324KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa umbali wa kilomita 5.267 katika uelekeo wa 163.032° hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P18 yenye majira - nukta 470750MS, 94397362KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa umbali wa kilomita 2.097 katika uelekeo wa 275.25° hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NP21 yenye majira - nukta 468653MS, 9397377KZ; baada ya

*Tangazo la Serikali Na. 281 (linaendelea)*

hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 3.898 katika uelekeo wa 170.10° hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NP yenye majira - nukta 467987MS, 9401218KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini pembezoni mwa mto Pangani kwa umbali wa kilomita 16.325 katika uelekeo wa 270.003° hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NP yenye majira - nukta 484108MS, 9402197KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 4.297 katika uelekeo wa 180.01° hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P89 yenye majira - nukta 483641MS, 9397893KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa umbali wa kilomita 3.183 katika uelekeo wa 82.26° hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba LA179 yenye majira - nukta 480485MS, 9397481KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 4.504 katika uelekeo wa 358.14° hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VTB yenye majira - nukta 480625MS, 9392928KZ hadi ulipoanzia".

Dodoma,
17 Machi, 2023

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*